SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO ZANZIBAR

BALOZI MOHAMED RAMIA ABDIWAWA (MBM)

KUHUSU MAPENDEKEZO YA BAJETI YA SERIKALI (MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI (BAJETI) YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.

I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naanza kwa kulitukuza jina la Mola wetu muumba na muweza wa kila kitu na kumshukuru kwa kutujaalia sote uhai, uzima na neema nyengine zilizotuwezesha kukutana tena leo hii. Kwa mara nyengine tunakutana ili kutimiza wajibu wetu muhimu kwa jamii tunayoitumikia na kuiongoza, unatokana na matakwa ya Kifungu cha 105 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 41(3) cha Sheria ya Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa vifungu hivyo, Waziri mwenye dhamana ya Fedha ana wajibu wa kutayarisha na kuwasilisha Baraza

la Wawakilishi Makadirio ya Bajeti ya mwaka unaofuata, kabla ya kumalizika mwaka wa Fedha. Kwa kuwa tuko ukingoni mwa mwaka wa Fedha wa 2018/19 nawasilisha Mapendekezo haya ya makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa 2019/2020 ili kutimiza matakwa hayo ya Kikatiba na Sheria.

3. **Mheshimiwa Spika,** Kwa sababu hiyo, na kwa heshima kubwa, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati Maalum ya kujadili Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

4. **Mheshimiwa Spika,** nimesimama hapa nikiwa Waziri wa Fedha na Mipango kufuatia kuteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais kushika dhamana hii muhimu kwa Serikali na nchi yetu kwa ujumla. Ni dhahiri kuwa, hii ni imani kubwa kwangu mimi kutoka kwa kiongozi wa nchi yetu na Mkuu wa Serikali. Namshukuru

sana Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa imani hiyo na kwa kuendelea kunisaidia na kunipa miongozo muda wote ambayo inarahisisha sana utendaji wangu.

5. **Mheshimiwa Spika,** Kubwa zaidi, namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake wa hekima, busara wenye subra kubwa, uweledi na uadilifu wa kupigiwa mfano. Kwetu sote tulio karibu na Mheshimiwa Rais, tuna fursa adhimu ya kujifunza mengi kutoka kwake kuhusiana na uongozi na maisha kwa ujumla. Serikali anayoiongoza imejenga imani kubwa kwa wananchi. Amani imeshamiri na hivyo nchi yetu inaendelea kuwahudumia watu wake kwa kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2015 – 2020 na MKUZA III.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa uzito huo huo pia namshukuru sana msaidizi wake mkuu, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa

Pili wa Rais, kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais na kwa msaada wake mkubwa kwetu Mawaziri wote na kwa uongozi wake imara wenye kutupa nguvu na kututia moyo wa utendaji. Mheshimiwa Balozi Seif ni nguzo yetu katika utendaji Serikalini na pia katika kutuongoza vyema na kutuunganisha hapa katika chombo muhimu kwa nchi yetu, Baraza hili lenye uwakilishi wa wananchi wote wa Zanzibar na makundi maalum. Ni kiongozi jasiri na asiyeyumba.

7. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ni mojawapo ya nchi mbili zilizoungana April 1964 na kuunda Jamhuri moja, ya Muungano wa Tanzania, nchi nyengine ikiwa ni Tanganyika, sasa Tanzania Bara. Mwaka huu tumeadhimisha kutimia miaka 55 ya Muungano wetu. Utulivu na Maendeleo ya kila katika Jamhuri yetu unategemea sana na utulivu wa pande zote mbili, mashirikiano yaliopo baina ya viongozi wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano na uongozi wetu wa

pamoja wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hakika Muungano wetu umeendelea kuwa ni wa mfano.

8. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara, usioyumba na wenye kujali kwanza maslahi ya Taifa letu na watu wake, hususan walio wengi ambao ni wanyonge. Kwake yeye tunafurahia muelekeo mpya na usiotetereka wa kuimarisha uwajibikaji katika sekta ya Umma, kupambana kidhati na vitendo vya rushwa na ubadhirifu na ulinzi wa mali za Taifa. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapata sifa kutoka kila pembe ya dunia kwa misimamo yake madhubuti.

9. **Mheshimiwa Spika,** wazee wetu waliotangulia walitufunza mengi kwa kutumia njia ya methali na kauli fupi zenye ujumbe mkubwa; ***misemo.***

Mojawapo wa misemo hiyo ni kuwa ***"Kidole kimoja hakivunji chawa".*** Ujumbe mkuu wa msemo huu ni msisitizo juu ya faida kubwa ya mashirikiano yanayopelekea kwa pamoja kufikia mafanikio makubwa zaidi kuliko kwa mtu mmoja mmoja.

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mashirikiano makubwa anayoyapata Mheshimiwa Rais kwa wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu, ni ushahidi wa faida za msemo huo. Kwetu sisi pia tunafarijika sana na mashirikiano hayo na nawapongeza sana Mama Samia na Mheshimiwa Majaliwa, kwa uongozi wao imara.

11. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia nitangulize pongezi kwa uongozi wa Baraza hili, chini ya unahodha wako, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid. Baraza limeweka viwango vipya kwa kuwatumikia wananchi na kuisimamia Serikali kwa heshima kubwa bila ya kutetereka.

    Mheshimiwa Spika, katika kikao hiki cha Bajeti kwa mfano, tumeshuhudia Waheshimiwa Wajumbe wakiibana kwa hoja Serikali, kwa niaba ya Wananchi wanaowawakilisha, na Serikali kulazimika kufanya kazi ya ziada ya kuyapatia majibu ya uhakika maswali ya Waheshimiwa Wawakilishi wa Wananchi. Ni dhahiri kuwa wananchi walifuatilia vya kutosha mijadala yetu. Sisi ni kitu kimoja na tutaendelea hivyo katika kuwatumikia wananchi wote.

12. **Mheshimiwa Spika,** hata hivyo haya yote yamefanyika katika hali ya kuheshimiana na bila ya kutumia lugha za kejeli, dharau au ufedhuli. Nakupongeza sana wewe Mheshimiwa Spika, Naibu wako Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na

wenyeviti wa Baraza, Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar. Hakika kazi yenu ni ngumu mno lakini mnaitekeleza kwa uweledi mkubwa. Hongereni sana.

13. **Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie shukrani na pongezi hizi maalum kwa kutambua na kuthamini mchango wa Taasisi mbili muhimu. Kwanza, ni Mhimili wetu wa tatu, wa kulinda Haki zetu sote; mhimili wa Mahkama. Chini ya Mfumo wetu wa Dola, Mhimili huu ndio unakamilisha Mihimili yetu mitatu ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi chote hiki tumeshuhudia ukimya na utulivu mkubwa katika Mhimili wa Mahkama. Hii ni ishara ya kuwa nako mambo yanakwenda vyema na wananchi wana imani kubwa na utendaji wa Mhimili huo. Hivyo, naomba nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Jaji Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar kwa kuuongoza vyema Mhimili huo.

14. **Mheshimiwa Spika,** taasisi ya pili muhimu ambayo naomba nayo niishukuru kwa dhati ni Ulinzi. Pamoja na jitihada za wananchi za kudumisha amani na utulivu, lakini tunafarijika sana na utendaji wa vyombo vyetu vyote vya ulinzi na usalama. Utendaji wao huo ndio unatufanya wananchi sote tuishi kwa amani, bila ya khofu na kuweza kufanyakazi na mambo yetu ya kijamii bila ya woga. Najua kuna vyombo vingi vinanvyosimamia ulinzi wetu, iwe katika kulinda mipaka yetu ndani ya nchi, vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Idara Maalum za SMZ, hivyo kwa ujumla wao nimeviita taasisi moja ya “Ulinzi”. Kwa niaba ya wananchi wote wa Zanzibar, naishukuru sana taasisi hii muhimu kwa ujumla wake. Zanzibar ni salama na Jamhuri ya Muungano yote ni salama.

15. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, pongezi na shukrani, naomba sasa uniruhusu nianze kwa kuwasilisha kwa mukhtasari mwenendo wa uchumi wetu kwa

mwaka 2018 na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha miezi tisa kilichoishia tarehe 31 Machi 2019.

II. MWENENDO WA UCHUMI WA ZANZIBAR

16. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya mwenendo wa uchumi wetu niliyawasilisha asubuhi ya leo wakati nikiwasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2018 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19. Naomba nieleze tena kiufupi tu kuwa Taarifa ya Utafiti wa Hali ya Uchumi na Kijamii ya mwaka 2018 inaonesha kuwa bado uchumi wetu umeendelea kuonesha ukuaji imara. Pato Halisi la Taifa kwa Zanzibar limeongezeka na kufikia TZS 2,874 bilioni kutoka TZS 2,684 bilioni lililoripotiwa mwaka 2017.

17. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza leo asubuhi, kuimarika kwa huduma za utalii ikiwemo kuongezeka kwa watalii waliotembelea

Zanzibar na muda wao wa kukaa nchini, kwa upande mmoja na mafanikio katika Kilimo ikiwemo uzalishaji wa mazao ya chakula na mwani, kwa upande mwengine, yamechangia sana katika ukuaji huu.

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa vigezo hivyo, uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika ambapo kwa kipindi hicho umekuwa kwa asilimia 7.1 ambao ni moja ya kasi kubwa za ukuaji wa uchumi miongoni mwa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara.

19. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Huduma imeendelea kuwa ndio tegemeo kuu la uchumi wetu. Kwa mwaka 2018, mchango wa Sekta hiyo katika Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 51.3 kutoka asilimia 48.6 ya mwaka 2017. Mchango wa Sekta ndogo ya malazi na Huduma za Chakula ndio umeongezeka zaidi kutoka asilimia 14.7 hadi asilimia 19.5. Hali hii imejitokeza kutokana na ukuaji wa kasi zaidi

kwa Sekta ya Huduma kutoka ukuaji wa asilimia 7.7 mwaka 2017 hadi 10.4 mwaka 2018.

20. Mheshimiwa Spika, tofauti na mafanikio hayo mazuri kwa Sekta ya Huduma, kasi ya ukuaji ilipungua kwa Sekta za Kilimo na Viwanda ambapo kwa Kilimo ilipungua kutoka asilimia 5.6 ya mwaka 2017 hadi 2.2 mwaka 2018, ikiathiriwa zaidi na kupungua kwa uzalishaji wa Karafuu. Kwa Viwanda, ukuaji ulifikia asilimia 3.7 mwaka 2018, ukiwa chini ikilinganishwa na asilimia 7.9 kwa mwaka 2017.

21. Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo ya tofauti ya ukuaji kwa Sekta ya Huduma kwa upande mmoja na za Kilimo na Viwanda kwa upande mwengine, kupanda kwa mchango wa Sekta ya Huduma kumeshusha ule wa Sekta za Kilimo na Viwanda katika Pato la Taifa. Kwa Kilimo, mchango wake mwaka 2018 ulikuwa ni asilimia 21.3 wakati mwaka 2018 ulikuwa asilimia 21.5. Katika kipindi hicho, mchango wa Sekta

ya Viwanda ulishuka kutoka asilimia 19.6 hadi asilimia 17.8.

A. Idadi ya Watu na Pato la Mwananchi

22. Mheshimiwa Spika, Kutokana na kuimarika kwa Pato la Taifa mwaka 2018, wastani wa kipato cha mtu mmoja mmoja nao umeongezeka kutoka TZS 2,104,000 sawa na Dola za Kimarekani 944 na kufikia TZS 2,323,000 sawa na Dola 1,026, kwa kuzingatia idadi ya watu 1,579,849 ambayo nchi yetu imekadiriwa kuwa nao katika mwaka 2018. Inatia moyo kuona kuwa wakati bado kunahitajika msukumo zaidi wa kuongeza uzalishaji na ukuaji wa Pato la Taifa, tunakaribia sana kufikia uchumi wa kipato cha kati cha USD 1040 kama lilivyo lengo la Dira ya Maendeleo ya mwaka 2020.

B. Mfumko wa Bei

23. Mheshimiwa Spika, eneo jengine muhimu kwa uchumi wowote hasa kwa uamuzi wa ama kuweka akiba au kuwekeza ni utulivu wa bei za bidhaa, huduma na sarafu. Kwa mwaka 2018, hali ya bei nchini imekuwa ya utulivu kwa kiwango cha kuendelea kuvutia uwekaji wa akiba na uwekezaji wa mitaji. Hali hii imedhihirika katika mfumko wa bei ambao umeendelea kuwa katika wigo wa tarakimu moja kwa wastani wa asilimia 3.9 ikimaanisha kuwa umepungua zaidi kutoka asilimia 5.6 wa mwaka 2017. Kwa upande wa bidhaa, utulivu huo umejitokeza zaidi katika chakula ambapo mfumko wa bei umeshuka kutoka wastani wa asilimia 5.5 hadi asilimia 1.4. Kwa bidhaa zisizo za chakula, mfumko umeshuka na kufikia asilimia 5.7 mwaka 2018 kutoka asilimia 5.8 mwaka 2017.

C. Thamani ya Shillingi ya Tanzania

24. Mheshimiwa Spika, Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani iliendelea kuwa tulivu kipindi chote cha mwaka 2018 ikilinganishwa na thamani ya sarafu za nchi nyengine duniani. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani ilipungua kwa wastani wa asilimia 1.6 ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka 2017. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa TZS 2,264 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,229 mwaka 2017. Kushuka kidogo kwa thamani ya shilingi kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi na kuimarika kwa Dola.

25. Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa kutia moyo wa utulivu wa bei ulichangiwa kwa kiwango kikubwa na kushuka kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia, hali nzuri ya hewa kwa uzalishaji wa bidhaa za chakula na jitihada za

Serikali na Benki Kuu kwa usimamizi wa Sera ya Fedha.

III. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (Julai - Machi) 2018/19

A. Makadirio ya mapato

26. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2018/19, Baraza lako tukufu liliidhinisha makadirio ya Serikali ya kukusanya jumla ya TZS 1.315 trilioni kwa mchanganuo ufuatao:

i. Jumla ya TZS 807.5 bilioni kutoka vyanzo vya ndani;

ii. Mapato ya Misaada kutoka Nje ya jumla ya TZS 464.2 bilioni, ikiwemo Ruzuku ya TZS 75.6 bilioni na Mikopo ya TZS 388.6 bilioni;

iii. Ruzuku ya TSZ 3.4 bilioni ya Mfuko wa pamoja wa wafadhili (Busket Fund); na

iv. Mikopo ya Ndani ya TZS 40 bilioni.

27. Mheshimiwa Spika, kati ya mapato ya ndani ya TZS 807.5 bilioni, jumla ya TZS 728.4 bilioni zitatokana na makusanyo ya vyanzo vya kodi na TZS 79.1 bilioni ni kutokana na vyanzo visivyo vya kodi kwa mgawanyo ufuatao:

a) Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) TZS 405.9 bilioni sawa na asilimia 50 ya makadrio ya mapato ya ndani;

b) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) TZS 301.5 bilioni sawa na asilimia 37 ya makadrio ya mapato ya ndani;

c) Mapato ya Mawizara TZS 70.1 bilioni sawa na asilimia 9 ya makadrio ya mapato ya ndani;

d) Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT TZS 21.0 bilioni sawa na asilimia 3 ya makadrio ya mapato ya ndani;

e) Gawio la faida kutoka Benki Kuu (BoT) TZS 4.0 bilioni sawa na asilimia 0.5 ya makadrio ya mapato ya ndani; na

f) Gawio la faida kutoka katika Mashirika ya SMZ TZS 5.0 bilioni sawa na asilimia 0.6 ya makadirio ya mapato ya ndani.

B. Utekelezaji halisi

28. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2018 hadi Machi 2019), ukusanyaji wa mapato umekuwa wa kuridhisha, japokuwa lengo la ukusanyaji halikuweza kufikiwa kwa sababu mbalimbali. Kwa ujumla, Serikali imemudu kukusanya jumla ya TZS 864 bilioni. Kati ya kiasi hicho, TZS 579.3 bilioni ni mapato ya ndani, sawa na asilimia 93.9 ya makadirio ya kipindi hicho ya kukusanya TZS 617.3 bilioni; TZS 247.5 bilioni ni Mikopo na Ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; TZS 32 bilioni ni mikopo ya ndani na Misaada ya kibajeti (GBS) yenye thamani ya TZS 6.4 bilioni.

29. Mheshimiwa Spika, ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka wa Fedha uliopita (2017/2018), kunajitokeza ukuaji wa mapato ya ndani kwa TZS 73.0 bilioni, sawa na asilimia 14.4, kutoka makusanyo ya TZS 506.6 bilioni. Kati ya makusanyo hayo, mapato ya kodi yalifikia TZS 512.6 bilioni sawa na asilimia 92.6 ya makadirio ya TZS 553.7 bilioni. Mapato hayo yamekuwa kwa asilimia 10.1 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka uliopita 2017/18 ambapo jumla ya TZS 465.3 bilioni zilipatikana. Mapato ambayo yamefanya vizuri zaidi kwa kuzingatia malengo yake ni mapato yasiyokuwa ya kodi ambayo yaliingiza TZS 66.7 bilioni, na hivyo kupindukia lengo kwa takriban asilimia 4.9.

30. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine muhimu yamefikiwa katika upatikanaji wa Ruzuku na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Mapato kutoka chanzo hiki yamefikia jumla ya TZS 247.5 bilioni ikiwa ni sawa na ongezeko

la asilimia 63.9 ikilinganishwa na makusanyo halisi kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2017/18 ya TZS 151.0 bilioni. Kiwango hicho cha utendaji kinatokana zaidi na kukwamuka kwa mradi wa umwagiliaji Maji unaofadhiliwa na Benki ya Exim ya Korea. Aidha, ilipokea Misaada ya kibajeti (GBS) yenye thamani ya TZS 6.4 bilioni katika kipindi cha mapitio.

31. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi wa Machi 2019, Serikali ilikopa jumla ya TZS 32 bilioni kutoka soko la ndani, sawa na asilimia 80 ya makadirio ya mwaka ya kukopa TZS 40.0 bilioni.

C. Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi

i. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

32. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, Mamlaka ya Mapato Tanzania - Zanzibar (TRA) ilikusanya jumla ya TZS 217.4 bilioni sawa na asilimia 97.4 ya

makadirio ya TZS 223.3 bilioni. Kati ya mapato hayo, Idara ya Forodha imekusanya TZS 109.0 bilioni, sawa na asilimia 88.3 ya lengo la kipindi hicho la TZS 123.5 bilioni na Idara ya Kodi za Ndani imekusanya TZS 108.4 bilioni sawa na asilimia 108.5 ya lengo la kukusanya TZS 99.8 bilioni.

33. Mheshimiwa Spika, utendaji wa Idara ya Forodha umeathiriwa na mwenendo wa biashara unaochangiwa na msongamano wa Makontena bandarini. Hali hiyo pia imepelekea mapato ya Idara ya Forodha kukua kwa takriban asilimia 2 tu ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 107.0 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka jana. Kinyume chake, mapato ya Idara ya Kodi za Ndani yalikua kwa asilimia 30 kutoka TZS 83.4 bilioni zilizokusanywa na Idara hiyo miezi tisa ya mwanzo mwaka 2017/18.

ii. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)

34. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mapitio, ZRB imekusanya jumla ya TZS 281.2 bilioni sawa na asilimia 89.4 ya makadirio ya kipindi hicho. Kutolipwa kwa wakati kwa marejesho ya Ushuru wa Bidhaa na Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa bidhaa zinazohaulishwa kutoka Tanzania Bara ya jumla ya TZS 17.0 bilioni na mabadiliko ya utozaji wa Kodi kwa huduma za Kampuni za Simu ndio sababu kuu kwa kiwango hicho cha utendaji kwa ZRB. Hata hivyo, pamoja na changamoto hiyo, mapato ya ZRB yameongezeka kwa asilimia 8.5 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 259.1 bilioni kwa kipindi kama hicho ya mwaka 2017/18.

iii. Mapato Yasiyokuwa ya Kodi

35. Mheshimiwa Spika, Serikali imemudu kukusanya jumla ya TZS 66.7 bilioni kutokana na mapato yasiyokuwa ya kodi, sawa na asilimia

104.9 ya lengo, kwa kipindi cha mapitio. Kiwango hicho cha ukusanyaji kimepelekea ukuaji wa asilimia 63.1 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana, ambapo TZS 40.9 bilioni zilikusanywa kutokana na kianzio hiki. Mwenendo huo mzuri umechangiwa na utendaji mzuri wa ukusanyaji katika Wizara mbalimbali, upatikanaji wa Gawio kutoka Mashirika ya SMZ lakini zaidi kupatikana Gawio la TZS 13.75 bilioni kutoka Benki Kuu, ikiwa ni ziada ya asilimia 343.8 dhidi ya makisio ya kukusanya TZS 4.0 bilioni.

iv. Kodi ya Mapato kwa Wafanyakazi wa SMT

36. **Mheshimiwa Spika,** Makusanyo ya Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar yalifikia TZS 14.0 bilioni sawa na asilimia 88.9 ya makadirio ya kipindi hicho.

v. Mapato ya Mfuko wa Miundombinu

37. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya mapato yaliyopokelewa kutokana na Mfuko wa Miundombinu kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019 yamefikia TZS 24.3 bilioni sawa na asilimia 61.7 ya makisio ya TZS 39.4 bilioni. Kati ya fedha hizo jumla ya TZS 17.0 bilioni zimekusanywa na ZRB sawa na asilimia 63.3 ya makadirio ya bajeti na TRA imekusanya jumla ya TZS 7.3 bilioni sawa na asilimia 58.3 ya makadirio ya bajeti. Upungufu huo wa mapato umetokana na kupungua kwa kasi ya uingizaji wa mizigo bandarini pamoja na upungufu wa mafuta ya petroli na diseli kulinganisha na matarajio.

IV. UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

38. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2018, Baraza la Wawakilishi liliidhinisha

marekebisho katika Sheria mbalimbali kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa Mapato ya Serikali. Mukhtasari wa utekelezaji wa hatua hizo ni kama ifuatavyo;

i. Marekebisho katika Ushuru wa Stempu

39. Mheshimiwa Spika, Baraza lako tukufu liliidhinisha marekebisho yafuatayo katika Sheria ya ushuru wa stempu nam. 7 ya mwaka 2017:

a. kufuta Ushuru Stempu kwa bidhaa za mchele na unga wa ngano ambazo pia zimesamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ili kumpa unafuu wa maisha mwananchi wa kawaida;

b. kufuta Ushuru wa Stempu kwenye tiketi za ndege zinazotolewa na Mashirika ya Kimataifa hapa Zanzibar kwa safari za nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuifanya Zanzibar ihimili ushindani; na

c. Kufuta Ushuru huo kwa uhaulishaji wa mali (Transfer of Property) bila ya malipo pale mali hizo zilizohaulishwa kwa taratibu wa mirathi au mume au mke wa ndoa anapompa mwenza wake kwa njia ya hiba.

Hatua zote hizo tayari zimeanza kutekelezwa tokea Julai 2018.

ii. Kuongeza Muda wa Kuwasilisha Ritani na Malipo ya Kodi

40. Mheshimiwa Spika, tayari Serikali ikerekebisha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA) nam. 7 ya mwaka 2009 kwa kuzichanganya tarehe za kuwasilisha ritani na kufanya malipo kuwa siku moja ya tarehe 20 ya mwezi unaofuatia wa mauzo.

Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi mwezi wa Julai, 2018.

41. Mheshimiwa Spika, Mbali na hatua hizo za kisheria, Serikali pia imechukua hatua za kiutawala zenye lengo la kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato. Miongoni mwa hatua hizo ni kama zifuatazo:

iii. Kutoa Muongozo wa Kodi ya Zuio (Withholding Tax Guideline)

42. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2018/19 Serikali ilipanga kutoa muongozo wa usimamizi na ukusanyaji wa Kodi ya Zuio (**Withholding Tax Guideline**) kwa Wizara, Idara na Taasisi mbali mbali za Serikali ili kuondoa kasoro zilizopo wakati wa kuzuia kodi ya Ongezeko la Thamani na Kodi ya Mapato. Wizara imefanya vikao na kutoa elimu na muongozo kwa Maafisa wa TRA, ZRB, Wahasibu na Wakaguzi wa hesabu za Serikali. Hatua hii imepelekea kukusanya jumla ya **TZS 27.7 Bilioni** kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, ambapo TRA imekusanya **TZS 19.6**

bilioni na **ZRB TZS 8.1 bilioni,** ikilinganishwa na **TZS 13.2 bilioni** (TRA imekusanya **TZS 7.1 bilioni** na **ZRB** ilikusanya **TZS 6.1 bilioni**) zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

iv. Kuimarisha Usimamizi wa Utoaji wa Leseni

43. Mheshimiwa Spika, Serikali iliweka mkakati wa kusimamia Mamlaka zote za utowaji wa leseni za biashara, ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuhakikisha kuwa leseni zote zinatolewa baada ya mfanyabiashara kusajiliwa na TRA na ZRB na kuonesha hati ya kutodaiwa kodi (Tax Clearence Certificate) kwa Taasisi hizo. Jumla ya mikutano 11 ilifanyika ambayo 7 kati ya hiyo ilifanyika Unguja na 4 Pemba kwa kuwajumuisha Madiwani, Maafisa mapato na Wakurugenzi wa Halmashauri za wilaya na Mabaraza ya Miji. Hadi kufikia Machi 2019 jumla ya **TZS 3.9 Bilioni** zimekusanywa kutokana na hatua hiyo.

v. Kufanya mapitio ya viwango vya Ada

44. Mheshimiwa Spika, Serikali ilikusudia kufanya mapitio ya viwango vya ada vinavyotozwa kutokana na utoaji wa huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali. Katika kutekeleza suala hili, Serikali imeanzisha zoezi maalum la kufanya uchambuzi kwa kupitia Wizara na Idara za Serikali ili kuainisha vianzio vyote vya mapato, ada na tozo zinazotumika, utaratibu wa ukusanyaji, Sheria na Kanuni zinazotumika katika ukusanyaji wa mapato pamoja na changamoto zinazopelekea kutokusanywa vizuri kwa mapato ya Serikali. Hadi kufikia Machi, 2019 Serikali imeshapitia jumla ya Wizara sita (6). Hatua hii imepelekea kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ambapo hadi Machi 2019 jumla ya **TZS 47.0 bilioni** zimekusanywa ikilinganishwa na **TZS 39.3 bilioni** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2017/2018.

V. MATUMIZI HALISI YA SERIKALI JULAI – MACHI 2019:

45. Mheshimiwa Spika, Kufikia Machi 2019 matumizi halisi yalifikia TZS 863.3 bilioni sawa na asilimia 83 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya matumizi hayo TZS 535.8 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 96 ya lengo na TZS 327.6 bilioni zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 68 ya lengo la kipindi cha mapitio. Mchanganuo wa matumizi halisi ya kazi za kawaida kwa kipindi cha miezi tisa ni kama ifuatavyo:

i. Malipo ya Mishahara

46. Mheshimiwa Spika, Serikali imetumia jumla ya TZS 247.7 bilioni katika kipindi cha mapitio kwa ajili ya kulipa mishahara kwa wafanyakazi wake. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kutumia TZS 247.5 bilioni. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya Mishahara kwa Wizara

na Taasisi za Serikali kupitia Mafungu (Votes) ni TZS 169.7 bilioni ambao ni sawa na asimilia 99 ya lengo la miezi tisa la kutumia TZS 171.4 bilioni. Mishahara kwa Taasisi zinazopokea Ruzuku ilifikia TZS TZS 78.0 bilioni, sawa na asilimia 102 ya makadirio ya TZS 76.5 bilioni.

ii. Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi

47. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, matumizi mengineyo (other charges) yalifikia jumla ya TZS 178.0 bilioni, sawa na asilimia 96 ya lengo la kutumia TZS 185.4 bilioni. Kati ya Fedha hizo, Wizara na Taasisi zenye Mafungu zilipatiwa jumla ya TZS 116.4 bilioni sawa na asilimia 96 ya lengo la kutumia TZS 121.25 bilioni. Matumizi haya yanaashiria ongezeko la asilimia 40 ikilinganishwa na matumizi halisi ya kipindi kama hicho cha mwaka 2017/18. Aidha, Tasisi zinazopokea Ruzuku zilipatiwa TZS 61.6 Bilioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya kutumia TZS 64.17 bilioni.

48. Mheshimiwa Spika, kupitia matumizi hayo ya fedha za ndani, Serikali imeendelea kutoa huduma za msingi kwa jamii yetu. Mfano wa maeneo ambayo yamenufaika na matumizi haya ni kama ifuatavyo:

a. Kuendelea kutoa huduma za afya bure nchini;

b. Ununuzi wa dawa ambapo serikali imetoa TZS 12.7 bilioni kama ilivyoahidi;

c. Kuimarisha huduma za hospitali ya Mnazi Mmoja na Hospitali nyengine nchini;

d. Kuhudumia matibabu nje ya nchi;

e. Kuendelea kutoa huduma ya elimu bure nchini, na bila ya michango kwa wazazi, kwa elimu ya maandalizi, msingi na Sekondari hadi Kidato cha Nne ikiwemo huduma za madaftari na gharama za mitihani;

f. Kugharamia mafunzo ya amali na kuendelea kutoa mikopo kwa elimu ya juu;

g. Kufanya matengenezo ya mtandao wa barabara nchini; na

h. Kutoa huduma nyengine mbalimbali kwa wananchi ikiwemo kuendesha shughuli za Baraza hili na Mhimili wa Mahakama kwa ufanisi mkubwa.

iii. Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu

49. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mapitio, jumla ya TZS 110.0 bilioni sawa na asilimia 88 ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 125.2 bilioni. Matumizi hayo yameelekezwa katika mambo yafuatayo:

a. Kulipia Mishahara na maslahi mengine kwa viongozi wakuu waliotajwa Kikatiba TZS 941 milioni;

b. Malipo ya Kiingua Mgongo na Pencheni TZS 25.1 bilioni;

c. Malipo ya Mikopo ya ndani na Riba TZS 18.7 bilioni; na

d. Matumizi mengine ya Serikali kupitia Mfuko Mkuu TZS 65.3 bilioni.

iv. Matumizi kwa Kazi za Maendeleo:

50. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, katika kipindi cha mapitio, matumizi kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo yalifikia jumla ya TZS 327.6 Bilioni sawa na asilimia 53.4 kwa makadirio ya mwaka ya kutumia TZS 613 bilioni. Kati ya kiasi hicho, matumizi kutokana na mapato ya ndani ni TZS 83.0 bilioni na kutokana na Mikopo na ruzuku kutoka nje ni TZS 244.6 bilioni. Maelezo ya kina ya matumizi katika kazi za Maendeleo nimeyatoa asubuhi hii wakati nikiwasilisha Utekelezaji wa

Mpango wa Maendeleo kwa kipindi hicho cha Miezi tisa.

v. Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu

51. Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Baraza lako tukufu watakumbuka kuwa mwaka 2015 Serikali ilanzisha Mfuko maalum wa Miundombinu kwa azma ya kuharakisha ujenzi wa miundombinu muhimu nchini. Matumizi haya ni sehemu ya matumizi kwa kazi za Maendeleo. Kwa kipindi cha mapitio katika mwaka wa Fedha unaoendelea, jumla ya TZS 39.5 bilioni zilikadiriwa kutumika kwa miradi mbalimbali kupitia Mfuko wa Miundombinu. Matumizi halisi katika kipindi hicho yamefikia TZS 23.2 bilioni, sawa na asilimia 59 ya makadirio ya mwaka mzima.

VI. MATARAJIO YA MAPATO JULAI – JUNI 2018/2019

A. Matarajio ya Mapato

52. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo ya mapato katika kipindi cha Julai 2018 hadi Juni 2019, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS 1,101.8 bilioni sawa na asilimia 83.8 ya makadirio ya mwaka. Kati ya matarajio hayo jumla ya TZS 790.8 bilioni ni mapato ya ndani sawa na asilimia ya 97.9 ya bajeti ya TZS 807.5 bilioni. Ukusanyaji huo utapelekea ukuaji wa mapato ya ndani kwa asilimia 14.8 ikilinganishwa na mapato halisi ya TZS 688.7 bilioni yaliyokusanywa mwaka uliopita. Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 261.2 bilioni ambapo ni sawa na asilimia 56.3 ya makadirio ya mwaka. Misaada ya kibajeti inatarajiwa kufikia jumla ya TZS 6.4 bilioni. Mfuko wa Pamoja wa wafadhili unatarajiwa

kufikia jumla ya TZS 3.4 bilioni na Dhamana za Hazina na Hatifungani zinatarajiwa kufikia jumla ya TZS 40 bilioni.

53. Mheshimiwa Spika, Mapato yakodiyanatarajiwa kufikia TZS 707.0 bilioni, sawa na asilimia 97.1 ya bajeti ya TZS 728.4 bilioni, yakimaanisha ukuaji wa asilimia 13.3 ikilinganishwa na mapato ya TZS 623.8 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita. Kitaasisi, ukusanyaji wa mapato ni kama ifuatavyo:

a. TRA - Zanzibar inatarajiwa kukusanya TZS 286.0 bilioni sawa na asilimia 94.9 ya lengo la kukusanya TZS 301.5 bilioni, na hivyo kupelekea ukuaji wa asilimia 11.7 ikilinganishwa na mapato ya TZS 256.0 bilioni yaliyokusanywa mwaka 2017/18.

b. ZRB inatarajiwa kukusanya TZS 400.0 bilioni kati ya makadirio ya TZS 405.9 bilioni, sawa na asilimia 98.5 ambapo ni sawa na ukuaji wa

asilimia 15.3 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato ya TZS 346.8 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita 2017/18.

c. Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT inatarajiwa kufikia TZS 21.0 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

54. Mheshimiwa Spika, Mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kuendelea kufanya vizuri zaidi na kufikia TZS 83.8 bilioni sawa na asilimia 105.9 ya bajeti ya TZS 79.1 bilioni, na kupelekea ukuaji wa asilimia 29.1 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato wa TZS 64.9 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita. Uchambuzi wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:

a. Mapato ya Mawizara ni TZS 63.1 bilioni sawa na asilimia 89.9 ya makadirio ya mwaka ya TZS 70.1 bilioni;

b. Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia TZS 6.9 bilioni sawa na asilimia 139.2 ya makadirio ya mwaka ya TZS 5.0 bilioni.

c. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia TZS 13.7 bilioni sawa na asilimia 343.8 ya makadirio ya mwaka ya TZS 4.0 bilioni.

Mfuko wa Miundombinu

55. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2018/19, matarajio ya mapato ya Mfuko wa Miundombinu ni kukusanya TZS 32.7 bilioni sawa na asilimia 82.5 ya makadirio. Kati ya Fedha hizo, TRA inatarajiwa kukusanya TZS 10.2 bilioni na ZRB inatarajiwa kukusanya TZS 22.5 bilioni.

B. Matarajio ya Matumizi Julai - Juni 2019

56. Mheshimiwa Spika, Hadi Juni 2019, matumizi ya Serikali kwa mwaka mzima yanatarajiwa

kufikia TZS 1.10 trilioni sawa na asilimia 83.8 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 1.315 trilioni. Kiwango hicho kinamaanisha ongezeko la matumizi kwa asilimia 22.5 ikilinganishwa na matumizi ya mwaka uliopita ya TZS 899.5 bilioni. Kati ya matumizi hayo, matumizi ya Kazi za Kawaida yanatarajiwa kufikia TZS 721.8 bilioni kwa mchanganuo ufuatao:

i. Mishahara inatarajiwa kufikia TZS 341.5 bilioni ambapo TZS 232.2 bilioni ni kwa Wizara na Taasisi zenye Mafungu, sawa na asilimia 99.9 ya bajeti ya mwaka na TZS 109.3 bilioni ni kwa Taasisi zinazopokea Ruzuku, sawa na asilimia 104.5 ya bajeti ya mwaka;

ii. Matumizi Mengineyo yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 231.9 bilioni ambapo kwa Wizara na taasisi zenye Mafungu ni TZS 148.6 bilioni sawa na asilimia 100.9 ya bajeti ya mwaka mzima na kwa Taasisi zinazopokea Ruzuku ni TZS 83.3 bilioni sawa asilimia 98.1 ya bajeti ya mwaka; na

iii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ya TZS 148.5 bilioni ambapo sawa na asilimia 100 ya bajeti ya mwaka iliyorekebishwa.

57. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya Mpango wa Maendeleo, matarajio ni kutumia jumla ya TZS 392.8 bilioni hadi Juni mwaka huu, sawa na asilimia 64 ya makadirio ya awali. Kati ya matumizi hayo, TZS 131.6 bilioni ni kutokana na fedha za ndani, sawa na asimilia 88.4 ya makadirio na TZS 261.2 bilioni ni Mikopo na Ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 56.2 ya makadirio ya TZS 464.2 bilioni.

VII. Deni la Taifa

58. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2019, Deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 57 na kufikia TZS 815.9 bilioni kutoka TZS 519.8 bilioni za Machi 2018. Deni la Ndani ni TZS 137.5 bilioni ambalo limeongezeka kwa asilimia

20 ikilinganishwa na TZS 114.4 bilioni la Machi, 2018. Kuongezeka huko kunatokana na madai mapya ya Kiinua mgongo kwa wastaafu na kuchukuliwa mikopo mipya kutoka ZSSF ya TZS 12.0 bilioni na Hati Fungani kupitia Benki Kuu ya TZS 22.5 bilioni. Ongezeko hilo linajitokeza pamoja na Serikali kulipa jumla ya TZS 25.1 bilioni la kiinua mgongo kwa wastaafu 1,286, Riba na Mikopo jumla ya TZS 18.72 bilioni na TZS 3.80 bilioni kwa wazabuni.

59. Mheshimiwa Spika, Deni la Nje limefikia TSZ 678.4 bilioni, deni hili limeongezeka kwa asilimia 88 hadi Machi, 2019 ukilinganisha na TZS 361.5 bilioni deni kwa nje kwa Machi 2018. Sababu ya kuongezeka Deni hilo ni kuingizwa fedha kiasi cha Dola 79.7 milioni kwa miradi inayoendelea sawa na TZS 181.8 bilioni pamoja na kufanya usuluhishi wa kimahesabu baina ya SMZ na SMT ulioingiza jumla ya Dola 56.1 milioni sawa na TZS 127.8 bilioni. Sababu nyengine ni athari ya kubadilika kwa thamani

ya Shilingi dhidi ya dola ya Kimarekani. Hata hivyo, Deni hili la Taifa ni sawa na asilimia 24 ya Pato la Taifa na hivyo, kwa kuzingatia vigezo vya kitaifa na kimatafia, bado linahimilika.

60. Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi wa Deni la Taifa, matumizi ya fedha hizo na tija yake ni muhimu sana ili kuinusuru nchi yetu na kuingia katika mzigo mkubwa kwa siku za usoni. Ni kwa sababu hii ndio Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, namba 12 ya mwaka 2016 ikaweka Sehemu maalum ya kumi, yenye Vifungu 13 kuanzia cha 58 hadi 70, kwa ajili ya masuala ya Mikopo na Usimamizi wa Deni, ikiwemo kuanzishwa kwa Kamati ya Kusimamia Deni chini ya Kifungu cha 59. Nina furaha ya kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa kwa Mamlaka niliyopewa chini ya Kifungu hicho, tayari nimeteua Kamati ya Kusimamia Deni (Zanzibar Debt Management Committee) inayoongozwa na Katibu Mkuu wa Hazina na inayosaidiwa na Kamati ya

Kiufundi ya Usimamizi wa Deni (Technical Debt Management Committee), inayoongozwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali. Ni matumaini yangu kuwa usimamizi wetu wa Deni la Taifa utaimarika zaidi kwa kuzingatia matakwa hayo ya Kisheria na kuanzishwa kwa Kamati hizo.

61. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kumalizia maelezo yangu ya tathmini ya utekelezaji kwa miezi tisa na matarajio ya kumalizia mwaka, naomba uniruhusu nieleze mambo machache yaliyosimamiwa na Serikali katika kipindi hichi na yenye umuhimu maalum. Nianze na taarifa kuhusu maendeleo ya ujenzi wa meli mpya ya mafuta, MT Ukombozi II.

62. **Mheshimiwa Spika,** tokea awali, Serikali iliamua kujenga meli mpya za abiria na mafuta ili kuchukua nafasi ya meli za MV Mapinduzi, meli ya abiria ambayo iliuzwa kutokana na uchakavu wake, na MT Ukombozi, meli ya Serikali ya mafuta ambayo tunalazimika kuiondoa kwenye

huduma kutokana na uchakavu lakini zaidi mahitaji ya sasa ya usalama wa meli za mafuta ambayo meli hii haiyatimizi. Wote tunafahamu kuwa meli ya MV Mapinduzi II imeshanunuliwa na inaendelea kutoa huduma muhimu kwa usafiri wa wananchi baina ya visiwa vyetu.

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa meli ya mafuta, nina furaha kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa ujenzi wa meli hiyo umekamilika huko Yichang, nchini China. Makabidhiano ya awali yanatarajiwa kufanyika mapema mwezi ujao mjini Shanghai baada ya ukaguzi wa wataalamu wetu na makabidhiano rasmi yatafanyika hapa Zanzibar baada ya kuwasili kwake ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2019/2020. **Kama ilivyokuwa kwa meli ya MV Mapinduzi II, meli ya MT Ukombozi II inajengwa kwa kutumia fedha zetu za ndani.**

64. **Mheshimiwa Spika,** Meli hiyo itagharimu Euro 14,324,000, sawa na TZS 37.1 bilioni.

Hadi sasa Serikali imelipa kwa wakati vipingili vinne vyenye jumla ya Euro 12,891,600, sawa na TZS 33.4 bilioni. Kwa sasa, kwa mujibu wa Mkataba, tumebakisha malipo ya kipingili cha mwisho ambacho kinapaswa kulipwa baada ya makabidhiano ya meli. Meli hiyo itakuwa na uwezo wa kuchukua Tani 4,500 za mafuta.

65. **Mheshimiwa Spika,** eneo jengine linalokhalisi kulieleza ni maendeleo ya ujenzi wa misingi ya maji ya mvua kupitia Mradi wa Huduma za Mijini (ZUSP) unaofadhiliwa kwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Sote ni mashahidi kuwa takriban maeneo mengi yaliyopangwa kujengwa misingi hiyo tayari yamekamilika na imesaidia sana kuwaondolea wananchi wa maeneo hayo adha ya mafuriko wakati wa mvua kubwa.

66. **Mheshimiwa Spika,** naamini wananchi wa maeneo ya Muembemakumbi, Kwamtipura, Sogea, Magomeni, na Mpendae, ni mashahidi wa mafanikio haya mema kwao. Kazi kubwa

inayoendelea sasa ni kumalizia eneo la Mwanakwerekwe na kuliunganisha na msingi uliopo Magogoni na kupitia Sebleni, Mikunguni, Saateni hadi pwani. Kazi hiyo pamoja na yakuiinua barabara ya Mwanakwerekwe na kuimarisha kingo za mabwawa ya Mwanakwerekwe na Sebleni nayo inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka ujao wa fedha.

67. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Serikali inatambua tatizo lililojitokeza katika eneo la Kilimani ambapo maji yanayoletwa na misingi miwili mikubwa mipya yanazidi uwezo wa msingi wa zamani na hivyo kuleta athari kwa wakaazi wa eneo hilo. Tatizo hili nalo litatatuliwa ndani ya mwaka ujao wa fedha kwa kujengwa msingi mpya wenye uwezo mkubwa zaidi katika eneo hilo hadi pwani ya Kilimani.

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa azma hiyo hiyo ya kuondelea shida wananchi na kuihami haiba ya Zanzibar, Serikali imejenga na kukamilisha

daraja jipya lenye njia mbili katika eneo la Kibonde Mzungu. Kwa miaka ya nyuma kumetokea maafa mara nyingi katika eneo hilo ikiwemo wananchi wenzetu kupoteza maisha. Kwa sasa eneo hilo linapitika muda wote. Serikali kwa sasa imeamua kuijenga upya, kwa njia mbili, barabara inayounganisha daraja hilo na Barabara mpya inayotoka Mwanakwerekwe hadi Fuoni. Tumetumia fedha zetu wenyewe.

69. **Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu, eneo la Kiembesamaki katika barabara inayokwenda Uwanja wa Ndege limekuwa ni kero kubwa kwa watumiaji wa barabara hiyo, wakiwemo wananchi na watalii wetu, kutokana na kutuwama kwa maji mengi. Hatimae tatizo hili nalo limepatiwa ufumbuzi baada ya kujengwa msingi mkubwa uliopitia Mbweni hadi pwani ya Mazizini. Miradi hii muhimu nayo imegharamiwa na fedha zetu wenyewe kutokana na mapato ya ndani.

70. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Serikali kupitia Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi, katika eneo la Gombani, Chake Chake Pemba. Jengo hilo lenye sehemu tatu zilizoungana, kwa sasa limetoa nafasi kwa Ofisi za Wizara sita huko Pemba kuwemo katika jengo hili. Maelezo ya kina ya jengo lenyewe yametolewa siku ya uzinduzi wake uliofanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tarehe 2 Mei mwaka huu. Ujenzi huu nao, pamoja na vifaa vyote vilivyoweka ikiwemo vya usalama umegharamiwa kwa fedha zetu za ndani.

71. Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe taarifa kwa Baraza lako tukufu kuhusu matokeo ya mazungumzo ya muda mrefu baina ya Serikali na Kampuni ya Zanzibar Telecom Plc Limited, maarufu Zantel, kuhusiana na matumizi ya Mkongo wa Taifa. Naelewa kuwa suala hili pia limejadiliwa mara kadhaa hapa Barazani.

Kwa mukhtasari, mwezi Februari mwaka 2013 Serikali iliingia Mkataba na Zantel ambao ulihusisha mambo yafuatayo kwa Kampuni hiyo:

a. kusimamia uendeshaji wa Mkongo huo na matengenezo yake;

b. kutumia baadhi ya njia za Mkongo huo kwa mawasiliano yake;

c. kuipatia Serikali kiwango cha STM 1 kwa ajili ya matumizi yake ya “internet”; na

d. Kuuza uwezo wa ziada kwa Kampuni nyengine kwa makubaliano ya serikali kupata asilimia 70 ya Mapato safi na Zantel kubaki na asilimia 30 iliyobaki.

72. Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya, Zantel imekuwa ikitumia Mkongo huo lakini haikuweza kuuza uwezo wa ziada na kulijitokeza

changamoto kadhaa za usimamizi wa Mkongo huo na hivyo Serikali kutopata mapato yake. Ili kurekebisha kasoro hiyo, Serikali ilianzisha mazungumzo na Zantel juu ya namna ya kufidia gharama za matumizi.

73. Mheshimiwa Spika, hatimae Serikali iliunda Kamati maalum ya Baraza la Mapinduzi, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, kuendesha majadiliano na Zantel. Serikali pia imeanzisha Wakala wake wenyewe wa kuuza uwezo wa mtandao wa Mkongo huo na kuondoa jukumu hilo kwa Zantel. Nina furaha kulijuilisha Baraza hili kuwa mazungumzo hayo na Zantel yamekamilika vyema na kwa kila upande kuridhika.

74. Mheshimiwa Spika, Mkataba wa makubaliano hayo umesainiwa tarehe 30 Mei 2019 sambamba na Mkataba mpya wa Matumizi ya Mkongo kwa Zantel. Chini ya Mkataba huo, mambo yafuatayo yamekubaliwa:

a. Zantel itailipa SMZ Dola 11.0 milioni kwa matumizi ya uwezo wa 39 STM 1 kwa kipindi hicho na cha ziada hadi Disemba 31, 2024;

b. Zantel itailipa SMZ Dola 220,000 kwa ajili ya kusaidia kujenga uwezo wa Wakala wa Serikali wa kusimamia Mkongo huo;

c. Zantel itailipa Serikali Dola 15,000 kila mwezi kwa ajili ya kugharamia uendeshaji na matengenezo ya Mkongo; na

d. Zantel itaipatia Serikali uwezo wa 3 STM 1 kwa ajili ya matumizi yake ya mawasiliano ya “internet”.

75. Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio makubwa, kwanza ya kumaliza mvutano baina ya Serikali na Zantel, Kampuni ambayo SMZ pia ni mwanahisa, pili kuwezesha kupatikana mapato kutokana na uwekezaji uliofanywa na Serikali na tatu kuwezesha Serikali kusimamia yenyewe ukodishaji wa uwezo wa ziada katika

mtandao huo kwa Kampuni nyengine za simu na mawasiliano.

76. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa namna alivolisimamia na kuliongoza suala hili nyeti, gumu na linalohitaji utaalamu mkubwa. Nampongeza pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ya Mawaziri na Watendaji na wataalamu wetu wote walioshiriki katika majadiliano hayo kwa kazi yao nzuri waliyoifanya kwa uzalendo mkubwa na hatimae ikazaa matunda mema; nasema well done!

77. Mheshimiwa Spika, Nawashukuru pia wawakilishi wa Kampuni ya Zantel kwa uwazi wao, nia ya kweli ya kumaliza tatizo hilo na kwa kuwezesha kufikiwa kwa makubaliano hayo.

78. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nieleze mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/2020.

VIII. MWELEKEO WA BAJETI, 2019/2020

79. Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa bajeti yetu kwa mwaka ujao wa fedha unatokana na shabaha zifuatazo:

80. Kuendelea kuwa na ukuaji imara wa Uchumi unaokadiriwa kufikia asilimia 7.8 kutokana na kuendelea kuimarika kwa uwekezaji wa umma na binafsi, kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa na huduma, kuimarika kwa tija katika uzalishaji na kuimarika zaidi kwa huduma za utalii nchini;

a. Uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa wa asilimia 24, ikiwa ni miongoni mwa kiwango cha juu cha jitihada za ukusanyaji mapato katika Kusini mwa Jangwa la Sahara;

b. Kuendelea kuwa na utulivu wa bei za bidhaa na huduma kwa kuwa na kiwango tarakimu moja cha Mfumko wa Bei;

c. Kuimarika kwa uwekezaji nchini na mazingira yake na hivyo kuongeza ajira kwa vijana; na

d. Kuendeleza utafutaji na uendelezaji wa rasilimali za Mafuta na Gesi Asilia.

81. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwakani itaendelea kuongozwa na malengo ya umaliziaji wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA III) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Bajeti pia italenga katika kutekeleza vipaumbele vya Taifa kama nilivyovitaja asubuhi ya leo wakati nikiwasilisha Mpango wa Maendeleo.

82. Mheshimiwa Spika, Kwa takriban miongo miwili sasa tumekuwa tukiongozwa na Mpango wetu wa Maendeleo wa muda mrefu, Dira ya Maendeleo ya 2020. Dira hiyo imetekelezwa tokea mwaka 2000 na inatarajiwa kukamilika muda wake baadae mwakani. Kwa sababu hii, na kwa sababu ya haja ya kuwa na Mfumo Mkuu wa kutueleekza katika Maendeleo yetu kwa muda mrefu ujao, Serikali kupitia Tume ya Mipango imeanza matayarisho ya Mpango mpya wa Maendeleo wa muda mrefu, Dira ya 2050. Tayari Kamati mbili zimeundwa, moja ya kutathmini utekelezaji wa Dira ya 2020 na nyengine ya kuandaa Dira hiyo mpya. Matarajio ni kukamilisha kazi hizo ndani ya mwaka ujao wa fedha ambapo Dira hiyo mpya inatarajiwa pia kuhusisha kuipeleka Zanzibar katika uchumi wa Mafuta na Gesi.

83. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya bajeti yamezingatia pia misingi mikuu ya Sera za bajeti kama ilivyoelezwa katika ya Sheria ya Usimamizi

wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016. Aidha, kwa mujibu wa matakwa ya Sheria hiyo, maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2019/2020, yalitanguliwa na Majukwaa ya Bajeti na Uchumi kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Hakika maandalizi haya yamenufaika sana na maoni na ushauri uliotolewa katika Majukwa hayo ambayo pia yamesaidia kufikisha malengo ya Serikali kwa Wizara, Idara na Tasisi za Serikali, Serikali za Mitaa na Washiriki wengine kutoka Sekta binafsi na Jumuiya za Kiraia.

84. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni za Baraza letu hili tukufu, mwelekeo wetu wa Bajeti uliwasilishwa katika Baraza hili la Wawakilishi mwezi Februari mwaka huu. Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako katika ukamilishaji wa mapendekezo haya ya Makadirio ya mapato na Matumizi kwa mwaka ujao wa Fedha.

IX. MAKADIRIO YA MAPATO

A. Mapato ya Ndani

85. Mheshimiwa Spika, Jumla ya TZS 976.5 bilioni zinakadiriwa kukusanywa kwa mwaka 2019/20 kutoka katika vyanzo vya ndani, sawa na ukuaji wa asilimia 23.5 ikilinganishwa na matarajio ya mapato ya TZS 790.8 bilioni kwa mwaka wa fedha 2018/19. Kati ya fedha hizo TZS 859.7 bilioni ni mapato yatokanayo na kodi ambapo ni sawa na ukuaji wa asilimia 21.6 ya matarajio ya mapato ya TZS 707.0 bilioni kwa mwaka wa fedha 2018/19. Mapato yasiyokuwa ya kodi yamekadiriwa TZS 116.8 bilioni ikiwa ni sawa na ukuaji wa asilimia 39.5 ikilinganishwa na matarajio ya makusanyo ya TZS 83.7 bilioni kwa mwaka wa Fedha 2018/19.

Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT ni TZS 21.0 bilioni

86. Mheshimiwa Spika, Mapato yasiyokuwa ya kodi yamekadiriwa kukusanya TZS 116.8 bilioni sawa na ukuaji wa asilimia 39.5 ikilinganishwa na matarajio ya mapato ya TZS 83.7 bilioni ambayo yanayojumuisha:

a. Makusanyo ya Mapato ya Mawizara ya TZS 99.3 bilioni;

b. Gawio la Mashirika ya Serikali ni TZS 8.0 bilioni; na

c. Gawio kutoka Benki kuu ya Tanzania la TZS 9.5 bilioni.

B. Mfuko wa Miundombinu

87. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2019/20, mapato kwa Mfuko wa miundombinu yamekadiriwa kufikia TZS 40.9 bilioni ambapo ZRB imekadiriwa kukusanya TZS 26.0 bilioni na TRA imekadiriwa kukusanya TZS 14.9 bilioni

C. Mapato ya Nje

88. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na nia yetu ya dhati ya kuharakisha kujitegemea, bado tutaendelea kushirikiana na Mataifa rafiki na Mashirika ya Kifedha na ya Kibinaadamu ya Kimataifa katika kugharamia Maendeleo yetu. Kwa mwaka wa fedha 2019/20, Serikali inatarajia kupokea jumla ya TZS 394.6 bilioni kutokana na Mikopo na Ruzuku kutoka nje ya nchi. Kati ya kiasi hicho, TZS 299.1 bilioni kinatarajiwa kutokana na Mikopo na TZS 95.5 bilioni ni Ruzuku. Serikali pia inatarajia kupokea TZS 8.3 bilioni kupitia Mfuko wa Wafadhili (Basket Fund). Kuhusu Misaada ya Kibajeti (GBS), bado Serikali haitaiingiza moja kwa moja katika makadirio yake ya mapato na matumizi. Badala yake, itaendelea kutumia utaratibu wa Kibajeti wa “100T” ili kukidhi haja ya matumizi pindi Misaada hiyo na mikopo iliyokwama ikipokelewa wakati wowote wa mwaka.

X. MAKADIRIO YA MATUMIZI

89. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka ujao wa Fedha (2019/2020), Serikali inakadiria kutumia jumla ya TZS 1.4194 trilioni. Kati ya kiasi hicho, matumizi kwa kazi za kawaida ni TZS 842.4 bilioni na TZS 577.0 bilioni ni kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Maendeleo.

90. Mheshimiwa Spika, Katika matumizi ya kawaida, jumla ya TZS 417.9 bilioni zinahitajika kwa ajili ya kulipa mishahara, posho zinazoendana na mishahara pamoja na michango ya lazima kwa ajili ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF). Kima cha mshahara kilichotengwa ni sawa na asilimia 42.7 ya mapato ya ndani na hivyo kimezingatia matakwa ya Kifungu cha 5(1)(d) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma kinachokataza matumizi ya mishahara na maslahi kwa wafanyakazi wa umma kuwa makubwa kwa kuzingatia uwezo wa kiuchumi. Naomba pia kulitaarifu Baraza lako tukufu kuwa

katika mwaka huu, Serikali inatarajia kufanya marekebisho ya mshahara kwa wafanyakazi wake wenye uzoefu ili kukamilisha mageuzi ya maslahi ya wafanyakazi.

91. Mheshimiwa Spika, inasisitizwa kuwa marekebisho hayo hayatakuwa kwa wafanyakazi wote bali wale tu waliotumikia miaka mingi ambao nyongeza zao zimetolewa kwa awamu mbili hadi sasa. Marekebisho hayo yatahusu pia makundi mengine ya wanaopokea mishahara Serikalini ambayo hayakunufaika na nyongeza za mishahara mara iliyopita, ***wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi.*** Jumla ya TZS 75.7 bilioni zimetengwa kwa ajili hiyo ya marekebisho ya mishahara, nyongeza za mwaka, upandishaji vyeo na ajira mpya.

92. Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia mapato ya ndani yanayotarajiwa ya jumla ya TZS 960.4 bilioni, matumizi hayo kwa ajili ya mishahara yataacha bakaa ya TZS 542.5 bilioni kwa ajili

ya matumizi mengine. Aidha, kati ya jumla ya mapato hayo yanayotarajiwa kutokana na vyanzo vya ndani, yamo mapato yaliyokasimiwa matumizi maalum (earmarked) na hivyo kutoweza kugawanywa kwenye matumizi mengine.

93. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2019/2020, mapato hayo yenye matumizi maalum yanatarajiwa kufikia TZS 108.7 bilioni kama ifuatavyo:

i. Mapato kwa ajili ya Mfuko wa Miundombinu, TZS 41.0 bilioni;

ii. Makusanyo yatakayobakia ZRB kwa mujibu wa Sheria ni TZS 18.6 bilioni;

iii. Mapato ya Mfuko wa Barabara TZS 15.1 bilioni;

iv. Ada ya Bandari kwa mchango wa madawati ni TZS 2.5 bilioni;

v. Ada ya Kuendeleza Ujuzi (SDL), TZS 16.9 bilioni kwa ajili ya Elimu ya juu na mafunzo ya amali;

vi. Marejesho kwa Idara ya Uhamiaji Zanzibar ya TZS 13.9 bilioni sawa na asilimia 25 ya makusanyo yao; na

vii. Ada ya Usalama ya Uwanja wa Ndege kwa ajili ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege TZS 650 milioni.

94. Mheshimiwa Spika, Baada ya kuondoa kiasi hicho cha TZS 108.7 bilioni zinabaki jumla ya TZS 433.8 bilioni ambazo ndio zina fursa ya kugaiwa kwa ajili ya matumizi ya kuendeshea Serikali (Other Charges), Ruzuku kwa Taasisi mbalimbali na kazi za maendeleo. Ugawaji wa fedha hizo umezingatia mambo ya ziada yafuatayo:

i. Maeneo ya vipaumbele vya Taifa kwa mwaka 2019/20;

ii. Maagizo maalum ya Serikali kwa mujibu wa vipaumbele vya Taifa, yakijumuisha;

a. Elimu bure hadi Sekondari.

b. Ununuzi wa Dawa za lazima (essential drugs).

c. Ujenzi wa jengo jipya la Mahkama Kuu.

d. Utekelezaji wa Matokeo kwa Ustawi (R4P)

iii. Maagizo yatokanayo na Majukwaa ya Bajeti na Uchumi;

iv. Maelekezo yatokanayo na mjadala wa Mkabala wa Bajeti wa mwaka 2019/2020 katika Baraza la Wawakilishi;

v. Programu na miradi ya kimkakati (Flagship Projects) iliyotajwa katika MKUZA III;

vi. Programu na miradi yote ambayo Serikali ina dhima (Commitment) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;

vii. Programu na miradi yote iliyokuwa haijakamilika utekelezaji wa shughuli zake kwa bajeti ya mwaka 2018/19; na

viii. Ilani ya uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya 2015-2020.

95. Mheshimiwa Spika, eneo jengine muhimu lililotolewa maelezo na Serikali mwaka jana na kuleta mjadala mkubwa katika kikao hichi kinachoendelea ni suala la Ajira kwa Vijana. Mwaka jana Serikali ilianzisha Programu maalum na ikatenga TZS 3.0 bilioni kwa madhumuni hayo. Kwa bahati mbaya, matayarisho ya maeneo yatakayonufaika na utaratibu wa utoaji wa fedha na usimamizi wake yalichelewa sana

na kupelekea kutolewa thuluthi moja tu ya fedha hizo katika miezi tisa ya awali.

96. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa suala la ajira kwa vijana wetu, bado Serikali itaendelea na Programu hiyo kwa mwaka ujao ambako itaiongezea TZS 2.0 bilioni zaidi ya mwaka unaomalizika. Aidha, ninafuraha kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa kutokana na ziara ya mafanikio ya Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein aliyoifanya Falme za Kiarabu mwanzoni mwa mwaka jana Serikali ya Abu Dhabi imekubali kusaidia katika kuondoa tatizo la ajira kwa vijana. Kupitia mfuko wake wa “Khalifa Fund”, Serikali hiyo imetenga jumla Dola Milioni 10 za kimarekani, sawa takribani TZS 23 bilioni, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, kuanzia 2019/2020. Ni imani yangu kuwa fedha hizo, Programu yetu ya Vijana na Mfuko wa Uwezeshaji kwa pamoja vitaisaidia sana jitihada zetu za kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu.

97. Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo hayo ya jumla, Serikali pia imefanya uamuzi maalum kwa miradi makhsusi kuhusiana na matumizi ya mwaka ujao wa Fedha. Kwanza ni kukamilisha malipo kwa ajili ya ujenzi wa meli ya mafuta ya MT Ukombozi II. Kwa mujibu wa Mkataba, bado Serikali inapaswa kulipa kipingili cha mwisho cha Euro 1,432,400, sawa na TZS 3.71 bilioni wakati meli hiyo itakapokabidhiwa.

98. Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa Waheshimiwa Wajumbe kila mara wamekuwa wakihoji juu ya ukamilishaji wa Mradi wa miaka mingi wa ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Abeid Amani Karume hapa Unguja. Mradi huu unafadhiliwa na benki ya Exim ya China na bado kuna mambo kadhaa yanayohitaji kutatuliwa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo Kikatiba ndio yenye wajibu wa kukopa nje ya nchi, na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Benki yake ya Exim. Mambo haya bado

hayajajulikana lini hasa yatakamilika. Hata hivyo, kutokamilika kwa ujenzi wa jengo hilo kuna athari kubwa ya kiuchumi, kijamii na hata kisiasa kwa Zanzibar.

99. Mheshimiwa Spika, kwa sababu hii, naomba kutoa taarifa katika Baraza hili kuwa Serikali imefanya uamuzi maalum juu ya umaliziaji wa ujenzi huo. Wakati jitihada za kufanikisha upatikanaji wa fedha za ziada kutoka Benki ya Exim zikiendelea, ***Serikali imeamua kuupa kipaumbele cha kwanza Mradi huo. Kwa azma hiyo, imeamua kuuendeleza na kuukamilisha Mradi huo kwa fedha zake za ndani ambapo imetenga jumla ya TZS 61 bilioni, sawa na Dola 27 milioni, katika Bajeti ya mwaka ujao wa Fedha.***

100. Mheshimiwa Spika, tayari mazungumzo na Mkadanrasi, Kampuni ya Beijing Construction and Engineering Company Ltd (BCEG) na Benki ya Exim ya China yamefanyika na kuafikiana

juu ya ukamilishaji wa Mradi ndani ya miezi 15 ijayo na utaratibu wa malipo kwa kipindi cha miaka mitatu. Matarajio ni kuwa Mkandarasi ataanza tena kazi ndani ya mwezi Julai mwaka huu.

101. Mheshimiwa Spika, Serikali pia inakusudia kuanza hatua kwa hatua utekelezaji wa miradi mingine muhimu ya ujenzi wa Hospitali mpya ya rufaa na kufundishia katika eneo la Binguni na bandari mpya ya Mpigaduri. Tunayafanya haya yote sio kwa sababu Serikali ina uwezo mkubwa sana wa kifedha, lakini ni kwa sababu miradi hii ina umuhimu wa pekee kwa jamii yetu, wananchi wana shauku kubwa ya maendeleo, na Miradi yenyewe ni sehemu ya ahadi za Chama Cha Mapinduzi kwa wananchi wa Zanzibar kupitia Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2015.

102. Mheshimiwa Spika, Wazee wetu walitufunza kuwa “Kupanga ni kuchagua”; sisi tumeichagua

miradi hiyo kuwa ya kipaumbele maalum. Kwa umauzi huu, tumelazimika pia kuacha kutekeleza miradi mingine kadhaa, ambayo pia ni muhimu, ili fedha zote zielekezwe katika miradi tuliyoipa kipaumbele cha kwanza.

A. Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu

103. Mheshimiwa Spika, Kupitia Mfuko wa Miundombinu, jumla ya TZS 41.0 bilioni zimekadiriwa kutumika katika kugharamia Miradi maalum ya maendeleo. Miradi inayotarajiwa kugharamiwa na Mfuko huo kwa mwaka 2019/20 ni kama inavyoonekana katika jadweli hapa chini:

104. Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia jumla ya matumizi ya TZS 1,419.4 bilioni, mapato ya ndani ya TZS 960.4 bilioni na Misaada kutoka nje ya TZS 394.6 bilioni pamoja na Mfuko wa Wafadhili (Basket Fund) wa TZS 8.3 bilioni, kunajitokeza nakisi ya TZS 56.1 bilioni. Ili kupunguza nakisi

hiyo, hatua kadhaa za kuimarisha mapato zitachukuliwa katika mwaka ujao wa fedha. Hatua zinazopendekezwa ni pamoja na hizi zifuatazo.

XI. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20.

105. Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukuwa hatua maalum za kuweka utulivu wa mfumo wa kodi nchini kama njia mojawapo ya kushajihisha uwekezaji na ulipaji kodi kwa hiari. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, sambamba na dhamira yake ya kuhakikisha kunakuwa na utulivu na kutabirika kwa mfumo wa kodi na hivyo kuvutia uwekezaji zaidi, bado ***Serikali haipendekezi kupandisha viwango vya kodi.*** Matarajio ni kuwa wananchi na Wafanyabiashara wetu watanufaika na uamuzi huu.

106. Mheshimiwa Spika, badala yake, Serikali itaendelea kuchukuwa hatua mbalimbali za kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kuhakiksha mapato yote ya Serikali yanakusanywa kwa ufanisi zaidi pamoja na kuziba mianya ya upotevu. Hata hivyo, hatua hizi haziathiri mabadiliko katika Kodi za Muungano kama zilivopendekezwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na Mheshimiwa Waziri wa fedha na Mipango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano tarehe 13 mwezi huu.

Miongoni mwa hatua zinazopendekezwa kuchukuliwa ni hizi zifuatazo:

i. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)

107. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa walipa kodi katika sekta ya hoteli juu ya kuwepo vigezo

viwili katika kusajiliwa kwenye wigo wa VAT. Kwa sasa, ili hoteli ipaswe kusajiliwa kwenye VAT lazima itimize kigezo cha kiwango cha mauzo ghafi yasiopunguwa TZS 30Milioni kwa mwaka pamoja na kigezo cha ziada cha kuwa na kiwango cha kutozea huduma za malazi kisichopunguwa USD100 kwa mgeni kwa siku. Hali hii imepelekea Hoteli nyingi kusajiliwa katika mfumo wa kulipia Ushuru wa Hoteli (Hotel Levy) badala ya VAT na kuleta malalamiko ya mzigo mkubwa wa kodi kwa kukosa kujirejeshea kodi ya VAT wanayolipa katika ununuzi.

108. Mheshimiwa Spika, ili kurekebisha kasoro hiyo, inapendekezwa kufuta sharti hilo la ziada la kiwango cha Dola 100 kwa mgeni kwa siku. Hata hivyo, ili kuhami mapato ya Serikali, ZRB itachukua hadhari juu ya udanganyifu unaofanywa na wenye mahoteli wa kuficha kiwango halisi wanachotoza wageni wao.

ii. Kutoza kodi kwa Wageni wanaolala kwenye vyombo vya Baharini

109. Mheshimiwa Spika, Kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikitoza kodi kwenye Hoteli na nyumba za kulala wageni kwa mujibu wa Sheria husika. Kutokana na kukua kwa Sekta ya utalii nchini, kumejitokeza baadhi ya meli na merikebu za kitalii zinazokuja Zanzibar na wageni hulala kwenye vyombo hivyo badala ya hoteli.

110. Mheshimiwa Spika, ili kuleta usawa katika ulipaji wa kodi bila ya kujali aina ya malazi anayotumia mgeni hapa nchini, Serikali inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Hoteli nambari 1 ya mwaka 1995, ili kuwaingiza katika wigo wa kodi wageni wanaolala katika vyombo vya baharini. Hatua hiyo inatarajiwa kuingizia Serikali jumla ya TZS 0.60 Bilioni.

iii. Kujumuisha Gari za Mizigo zenye uwezo wa kubeba chini ya Tani moja katika utaratibu wa Ushuru wa Stempu.

111. Mheshimiwa Spika, imebainika kuwa wananchi wengi wanatumia gari za chini ya tani moja na nusu kuchukulia bidhaa kwa njia ya biashara. Awali gari hizo hazikuingizwa katika mfumo wa malipo wa Ushuru wa Stempu hazikuruhusiwa kuchukua mizigo.

112. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Barabarani nam. 7 ya mwaka 2003 ili kuzitambua na kuzisajili gari zenye uwezo wa kubeba mizigo chini ya tani moja zinazojishughulisha na biashara. Marekebisho ya Sheria hiyo yatapelekea pia kufanyia marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu nam. 7 ya mwaka 2017 ili kuziingiza gari hizo katika wigo wa kodi na kulinda mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajiwa kuingizia Serikali jumla ya **TZS 0.8 bilioni.**

vi. Hatua za Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi

113. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2019/20, Serikali inatarajia kuchukua hatua kadhaa za kiutawala ili kupunguza gharama pamoja na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya ndani kama ifuatavyo:

i. Kumarisha mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato katika Wizara na Taasisi za Serikali

114. Mheshimiwa Spika, Serikali katika kuhakikisha inaimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi (Ada na Tozo) kutoka katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali inakusudia kuweka mfumo maalum wa malipo kupitia benki (Revenue Gateway) utaorahisisha malipo kwa njia tofauti ikiwemo mitandao ya simu, wakala wa Benki ya PBZ au kupitia benki ya PBZ moja kwa moja. Hatua hii inatarajiwa

kuongeza ufanisi wa usimamizi na kupelekea kuongezeka mapato yasio ya Kodi kwa **TZS 3.0 Bilioni.**

ii. Kuimarisha Usimamizi na Ufuatiliaji wa Mapato

115. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia ZRB na TRA itaendelea kuhakikisha kwamba inaimarisha mifumo ya usimamizi wa mapato kwa kuoanisha mifumo iliyopo baina ya taasisi za ukusanyaji wa mapato na taasisi nyengine za Serikali ili kupata taarifa zaidi za walipakodi. Kufanya uhakiki zaidi wa ritani na nyaraka mbalimbali zinazowasilishwa na walipa kodi, kufanya ukaguzi kwa walipa kodi ili kuhakikisha kodi sahihi inalipwa, kusajili walipakodi zaidi pamoja na kutoa elimu zaidi ya kodi ili kuongeza uwajibikaji kwa walipa kodi na wananchi kwa ujumla. Hatua hii inatarajia kuiongezea Serikali jumla ya **TZS 7.11 bilioni** (TRA **TZS 4.06 bilioni** na ZRB **TZS 3.05 Bilioni**).

iii. Kugomboa madeni ya walipakodi

116. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2019/20, Serikali inakusudia kuweka utaratibu maalumu wa kugomboa madeni ya kodi ambao utahusisha kusamehe malimbikizo ya adhabu (Penalty) na riba (Interest) kwa kiwango cha asilimia 100 kwa walipakodi waliopo ZRB wenye madeni. Msamaha huo utatolewa kwa kipindi cha miezi sita kuanzia 1 Julai, 2019 hadi 31 Disemba, 2019. Hatua hii inatarajiwa kukusanya malimbikizo ya madeni ya kodi ya jumla ya **TZS 4.6 bilioni.**

iv. Kuongeza muda na ufanisi wa Utoaji na Usafirishaji wa Mizigo kupitia Bandarini

117. Mheshimiwa Spika, Kwa muda mrefu sasa wafanya biashara wamekuwa wakilalamika juu ya changomoto ya ucheleweshaji wa utoaji na usafirishaji wa mizigo kutokana na mrundikano wa mizigo katika bandari ya Zanzibar jambo

ambalo limekuwa likiwaongezea gharama katika uendeshaji wa biashara zao na kupunguza kasi ya ukusanyaji wa mapato. Katika kuhakikisha kwamba bidhaa zinatolewa na kusafirishwa bila ya kuchelewa, Serikali imeanzisha utaratibu wa kutoa huduma zote za utoaji na usafirishaji wa mizigo Bandarini kwa saa ishirini na nne (24). Ikitumiwa vyema, hatua hii itasaidia:

a. kukuza shughuli za kiuchumi nchini;

b. kuondoa mrundikano wa makontena bandarini;

c. kufanikisha biashara zaidi kutokana na bidhaa kuingia, kutolewa na kusafirishwa kwa haraka zaidi; na

d. kuimarisham mapato ya Serikali na wahusika wa bandari.

Ninawaomba wafanyabiashara nao kutimiza wajibu wao na kutoa mashirikiano kwa Serikali na kuwataka wasiongeze bila ya sababu za msingi gharama za nauli na nyenginezo zinazowaongezea ukali wa maisha watumiaji.

v. Kuwajengea uwezo watumiaji wa Mfumo wa Forodha (TANCIS)

118. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajia kuandaa mpango maalum wa kuwajengea uwezo wadau wanaotumia mfumo wa Forodha wa TANCIS. Miongoni mwa walengwa wakuu ni mawakala wa Forodha na wafanyakazi wa Shirika la Bandari, ili kuongeza ufanisi na weledi wa kufanya kazi za Forodha wakati wa kuingiza mizigo nchini na wakati kusafirisha bidhaa kwenda nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yanayotokana na biashara ya Kimataifa kwa upande mmoja na kupunguza gharama za kufanya biashara na kuchochea

kasi ya mzunguuko wa biashara kwa upande wa pili.

vi. Kupunguza mianya ya kuepuka kodi (Tax avoidance)

119. Mheshimiwa Spika, Bado kuna baadhi ya walipakodi ambao wanatumia njia za kisasa za kuepuka kulipa kodi bila ya kuvunja sheria. Kama ilivyo kwa ukwepaji, uepukaji wa kodi nao japo sio uhalifu lakini pia unapunguza makusanyo ya kodi. Ili kukabiliana na njia hizo, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka ya Mapato Tanzania itawajengea uwezo wafanyakazi wa idara ya kodi za ndani katika nyanja za uhaulishaji wa bei (transfer pricing) na utozaji wa kodi ya mapato kwa makampuni yanayofanya biashara katika mataifa mbali mbali (international taxation).

vii. Ushajihishaji wananchi kudai risiti za kielektroniki

120. Mheshimiwa Spika, utaratibu wa utoaji wa risiti kwa mfumo wa kieletrokiki unategemewa kuanza katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kwa lengo la kushajihisha Wananchi kudai risiti hizo, Bodi ya Mapato Zanzibar itaandaa utaratibu wa utoaji zawadi. Tunatanabahisha pia kuwa kama ilivo kwa mfanyabiashara asietoa risiti katika mauzo, mwananchi asiechukua risiti pia anatenda kosa la jinai. Hivyo tunawakumbusha wananchi watakaonunua bidhaa wasijiingize katika matatizo yanayoepukika. Wote wadai risiti na kusaidia kodi yao ifike Serikalini ili nayo iwahudumie kwa huduma zilizo bora zaidi.

viii. Mapitio ya Sheria na Kanuni zinazotoa Misamaha

121. Mheshimiwa Spika, eneo jengine muhimu linalotajwa kupoteza mapato ya Serikali ni

misamaha ya kodi, hasa pale inapotumiwa vibaya. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali itazifanyia mapitio Kanuni za vigezo vya misamaha ya kodi zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar ili ziweze kuendana na hali halisi ya mahitaji ya misamaha hiyo kwa sasa pamoja na kuziba mianya iliyojitokeza katika usimamizi. Aidha, ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo, kwa mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Serikali inakusudia kuangaliwa uwezekano wa kutumia miongozo ya Umoja wa Mataifa katika utoaji wa misamaha kwa Miradi ya Maendeleo (UN Guidelines on the Tax Treatment of ODA Projects) baada ya marekebisho, ikibidi. Misamaha itatolewa tu kwa ile inayotimiza masharti ya Sheria na yenye ulazima ka manufaa ya jamii yetu.

ix. Mapitio ya Tozo Mbalimbali kwa Kuimarisha Mazingira ya Biashara

122. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/20 Serikali inakusudia kufanya mapitio ya tozo na ada zinazotozwa katika sekta ya biashara, viwanda na huduma kwa lengo la kuimarisha mazingira ya biashara na kushajihisha ongezeko la usajili wa wafanyabiashara kuingia katika mfumo rasmi, hivyo kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato pamoja na kushajihisha ulipaji wa kodi, tozo na ada kwa hiari. Hatua hii pia itaondoa migongano ya majukumu ya kiutendaji baina ya Mamlaka za utoaji leseni, vibali na ruhusa nyengine na Mamlaka za Usimamizi.

123. Mheshimiwa Spika, maeneo yatakayozingatiwa katika mapitio ya tozo na ada hizo kwa kushirikiana na Sekta husika ni pamoja na haya yafuatayo:

a. Tozo za utoaji za leseni, vibali na ruhusa za kuendesha biashara, viwanda na huduma zinazotozwa na Wizara, Mamlaka za leseni na Serikali za Mitaa.

b. Tozo za usajili wa wafanyabiashara, majengo ya biashara, maghala na bidhaa.

c. Tozo za usajili na ukaguzi wa viwanda, maduka na bidhaa kwa ajili ya kulinda ubora, usalama na matumizi ya kemikali.

d. Tozo za ukaguzi wa ubora na usalama kwa bidhaa wakati wa usafirishaji na uingizaji.

e. Tozo za usafirishaji wa mwani, dagaa na mazao ya biashara.

f. Tozo nyengine za leseni, vibali na ruhusa zinazoathiri uendeshaji wa biashara, uwekezaji, viwanda na huduma.

x. Kuimarisha Usimamizi wa Ardhi

124. Mheshimiwa Spika, Serikali karibuni imefanya utafiti juu ya visiwa vyote vidogo vinavyoizunguka Zanzibar na ripoti ya awali imetolewa. Kutokana na matokeo hayo ya awali, Tume ya Mipango na Kamisheni ya Ardhi zimepewa maelekezo makhsusi ya kukamilisha kazi ya ziada. Matokeo ya kazi hiyo yamepelekea uamuzi wa Serikali kufanya mambo yafuatayo katika usimamizi wa Ardhi:

a. Kupitia upya viwango vya ukodishaji wa Ardhi (Lease Rent); na

b. Kupitia upya mikataba yote iliyokwisha kutolewa ya ukodishaji wa visiwa au sehemu yake.

Kwa sasa Serikali imesitisha ukodisha wa maeneo katika visiwa hadi hapo itakapotoa maelekezo mengine. Kazi zote hizo zinatarajiwa kukamilika katika mwaka ujao wa Fedha.

125. Mheshimiwa Spika, matarajio ni kuwa hatua hizi za kuimarisha mapato zitaiingizia Serikali jumla ya TZS 16.1 bilioni, ikiwemo TZS 13.1 bilioni katika hatua za kuimarisha mapato ya kodi na TZS 3.0 bilioni kwa hatua katika mapato yasiyo ya kodi. Mapato hayo ya ziada yatapunguza nakisi ya Bajeti na kubakisha nakisi ya TZS 40.0 bilioni. Serikali inapendekeza kukopa kiasi hicho cha Fedha katika soko la ndani ili kuleta uwiano wa mapato na matumizi.

Mwelekeo wa Mapato ya Ndani Kitaasisi

126. Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hizo, mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 976.5 bilioni. Kati ya makadirio hayo, TRA imekadiriwa kukusanya TZS 350.2 bilioni sawa na ukuaji wa asilimia 22.4 ikilingaishwa na matarajio ya makusanyo TZS 286.0 bilioni ya mwaka 2018/19. Kati ya mapato hayo, Idara ya Forodha imekadiriwa kukusanya jumla ya TZS179.2 bilioni na Idara ya kodi za

Ndani TZS 171.0 bilioni. Makisio hayo Kiidara yanamaanisha matarajio ya ukuaji wa asilimia 20.1 na asilimia 25.0 kwa Idara hizo.

127. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) imekadiriwa kukusanya TZS 488.5 bilioni sawa na ukuaji wa asilimia 22.1 ikilinganishwa na matarajio ya mapato ya TZS 400.0 bilioni kwa mwaka unaoendelea wa Fedha. Aidha, kama nilivyoeleza awali, mapato yasiokua ya kodi yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 116.8 bilioni na Kodi ya Mapato kwa Wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar ni TZS 21.0 bilioni.

XII. SURA YA BAJETI

128. Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia makadirio ya mapato na matumizi niliyoyawasilisha, Bajeti ya mwaka 2019/20 inatarajiwa kuhusisha mapato ya jumla ya TZS 1,419.4 bilioni. Kati ya fedha hizo:

a. Mapato ya ndani ni TZS 976.5 bilioni;

b. Ruzuku na Mikopo kutoka nje ni TZS 394.6 bilioni;

c. Ruzuku ya TZS 8.3 bilioni ya Mfuko wa Wafadhili (BF); na

d. Mikopo ya Ndani ni TZS 40.0 bilioni.

129. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa matumizi, jumla ya TZS 1,419.4 bilioni zinatarajiwa kutumika kama ifuatavyo:

i. Matumizi ya Kazi za Kawaida TZS 842.4 bilioni, na

ii. Matumizi kwa kazi za Maendeleo ni TZS 577.0 bilioni.

130. Mheshimiwa Spika, Kwa sura hii ya Bajeti, kunajitokeza taswira ifuatayo:

i. Mapato yetu ya ndani ya TZS 976.5 bilioni yatakidhi haja ya kugharamia matumizi yetu yote ya kazi za kawaida ya jumla ya TZS 842.4 bilioni;

ii. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, kulingana na matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, utagharamiwa na vyanzo vifuatavyo vya fedha:

a) Mapato ya Ndani ya TZS 93.1 bilioni;

b) Mfuko wa Miundombinu TZS 41.0 bilioni;

c) Mikopo kutoka nje TZS 299.1 bilioni;

d) Ruzuku kutoka nje TZS 95.5 bilioni, na

e) Mikopo ya Ndani ni TZS 40.0 bilioni.

Mfumo kamili wa Bajeti kwa mwaka 2019/2020 ni kama unavyonekana katika jadweli hapa chini.

131. Mheshimiwa Spika, tumekuwa na kawaida ya kueleza hali ya utegemezi kulingana na Mfumo wa Bajeti yetu. Kiwango cha utegemezi kimekuwa kikiangalia uwiano wa Ruzuku kutoka Nje na jumla ya Bajeti. Kwa bahati, makadirio ya mwaka 2019/2020 yanaashiria kukuwa kwa Ruzuku kwa TZS 19.9 bilioni kutoka TZS 75.6 bilioni zilizotarajiwa mwaka unaomalizika hadi TZS 95.5 bilioni kwa mwaka ujao wa fedha, sawa na ukuaji wa asilimia 26.3.

132. Mheshimiwa Spika, wakati kwa upande mmoja hali hii inamaanisha kuendelea kukubalika kwetu na mataifa rafiki na mashirika ya fedha ya kimataifa, kwa upande mwengine imebadilisha kidogo mwenendo wetu wa kuimarisha kujitegemea. Kwa makadirio hayo, kiwango cha utegemezi kitapanda kidogo mwaka ujao

wa fedha kutoka asilimia 5.7 iliyofikiwa katika mwaka unaoendelea hadi asilimia 6.7 katika mwaka ujao. Hata hivyo, bado kiwango hicho ni cha chini na cha kutia moyo sana.

XIII. SHUKURANI

133. Mheshimiwa Spika, uwasilishaji wa makadirio haya ni matokeo ya kazi kubwa na iliyohusisha watu wengi, wa taasisi tofauti na ngazi mbalimbali. Nna deni la shukrani kwao wote. Naomba nianze kwa kumshukuru tena Mheshimiwa rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa miongozo na dira yake iliyosaidia sana maandalizi haya. Ni kutoka kwake ambapo tumeweza kuwa na vipaumbele bayana vya maendeleo yetu na hivyo ugawaji wa fedha za bajeti. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

134. Mheshimiwa Spika, kwa mara nyengine namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Pili wa

Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa usimamizi wake na uratibu wa shughuli zote za Serikali katika maandalizi ya Bajeti hii. Nakushukuru wewe **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Naibu wako Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar na Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma kwa kazi kubwa ya kukiendesha kikao hiki cha bajeti kwa umakini unaohitajika. Muda wote nyie viongozi wetu hamkuyumba na Baraza hili nalo limepata utulivu mkubwa.

135. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Baraza, kabla ya kuwasilishwa katika Baraza zima, mapendekezo haya hupitiwa kwanza na Kamati ya Kudumu ya Bajeti. Naomba nishuhudie kwako kwamba kamati hiyo imefanya kazi kubwa sana na kwa upeo mkubwa wa uelewa na mashirikiano. Kwa dhati kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya

Kudumu ya Bajeti ya Baraza lako hili kwa kazi yao na mashirikiano.

136. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, tunazishukuru Kamati zote za Baraza lako na Waheshimiwa wajumbe wote kwani wao kwa ujumla wao wamefanikisha uidhinishaji wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara zote za Serikali na kuwezesha leo hii kuwasilishwa kwa Makadirio haya ya jumla ya Serikali. Wamehoji, wametaka maelezo ya ziada, wamezuia Shilingi lakini hatimae walikubaliana na Serikali na kuiruhusu iendelee na shughuli zake kwa matumaini ya kutekelezwa yale waliyoyasimamia. Huu ndio wajibu mkubwa wa Wawakilishi wa wananchi katika mfumo wa Demokrasia ya Uwakilishi.

137. Mheshimiwa Spika, maandalizi haya kwa kiasi kikubwa yamehusisha Watendaji, wakiongozwa na Kiongozi wa Utumishi wa Umma, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu

Kiongozi. Nachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi. Nawashukuru pia Makatibu Wakuu na watendaji wote walioshiriki katika kutayarisha makadirio haya. Hakika sote tumefaidika sana na kazi yao kubwa waliyoifanya, na tunaitambua na kuithamini. Aidha, katika kipindi cha maandalizi ya bajeti hii serikali imepata pigo kubwa kwa kuondokewa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda Ndugu Juma Ali Juma aliefariki tarehe 30 Aprili 2019 tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marahemu pahali pema peponi, Amiin

138. Mheshimiwa Spika, vinara wa uongozi na uandaaji wa makadirio haya wamo katika Wizara yangu, Fedha na Mipango. Namshukuru na kumpongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Bwana Khamis Mussa Omar, aliekuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango - Bwana Juma Hassan Reli ambae sasa

ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Biashara na Viwanda, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango - Bwana Iddi Haji Makame, Mhasibu Mkuu wa Serikali - Bi Mwanahija Almas Ali, na aliekuwa Kamishna wa Bajeti ambae sasa ni Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango – Bwana Mwita Mgeni Mwita.

139. Mheshimiwa Spika, kupitia kwao, nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara, Tume ya Mipango na Taasisi zilizo chini ya Wizara hususan Mamlaka ya Mapato (TRA) na Bodi ya Mapato (ZRB) kwa mchango wao mkubwa. Nawapongeza sana Bwana Juma Reli na Bwana Mwita Mgeni kwa uteuzi wa karibuni na nawatakia utumishi mwema katika nafasi zao mpya. Pongezi maalum pia ziende kwa Wakala wa Serikali wa Upigaji Chapa (ZAGPA) na wote waliofanikisha hadi vitabu vya Hotuba hii vikatoka kwa wakati.

140. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii haiwezi kukamilika bila ya kutambua na kushukuru mashirikiano na msaada mkubwa tunaoupata kutoka nchi rafiki na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa. Kwa muktadha huo, nashukuru sana nchi za Bahrain, Canada, Cuba, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Jamhuri ya watu wa China, Hispania, Indonesia, Israel, Itali, Korea ya Kusini, Kuwait, Malaysia, Marekani, Misri, Norway, Oman, Saudi Arabia, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Uturuki.

141. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mashirika, aidha, nashukuru sana msaada na mashirikiano na mashirika ya: ACBF, ACCRA, AfDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL, CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM Bank ya China, EXIM Bank ya Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMF, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, MCC, NORAD, OFID, ORIO-Netherlands, PRAP, SAUDI

FUND, Save the Children, SIDA, UNAIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, WB, WHO, WFP na WSPA.

XIV. HITIMISHO:

142. Mheshimiwa Spika, kwa mara nyengine nakushukuru sana kunipatia nafasi ya kutimiza wajibu wangu wa Kikatiba kama waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha. Fursa hii imeniwezesha kuwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka ujao wa Fedha, mwaka 2019/2020.

143. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu 2019/2020, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato ya Serikali ya kukusanya jumla ya Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia nne na Kumi na Tisa na Milioni Mia Nne (TZS 1.4194 Trilioni). Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani ni TZS 976.5

bilioni na Ruzuku na Mikopo kutoka Nje ni TZS 394.6 bilioni na TZS 40.0 bilioni ni mikopo ya ndani na TZS 8.3 bilioni ni Ruzuku ya mfuko wa pamoja wa wafadhili.

144. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, kwa mwaka huu wa 2019/2020, nina heshima ya kuliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nne na Kumi na Tisa na Milioni Mia Mia Nne (TZS 1.4194 Trilioni). Kati ya matumizi hayo, TZS 842.4 bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS 577.0 bilioni kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

145. Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa,
WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO,
ZANZIBAR.
20 JUNI 2019.